# MAFUNDISHO YA BIBLIA
## kwa WATOTO wa KANISA LA ELOHIM (COG)
**SikuYa Saba (7th day)**
**Robo Ya Nne 2023**
**Ya**

**OKTOBA , NOVEMBA na DESEMBA**
**Kutumiwa na Biblia**
**Watenda kazi wanahitajika, Mavuno ni mengi, Lakini watenda kazi ni wachache...**

**Tuma maombi yote kwa,**

**3RD ANGEL MESSENGER**

**S.L.P. 9774 NAKURU.**

**3rdangelmessenger@gmail.com**

**SIMU: +254 721576325/+254 780976325**

## SOMO LA WATOTO LA OKTOBA 7, 2023

## DHAMBI

**Somo kuu : Warumi 6:1-23**
**Fungu la kukariri : 1 Yohana 3:4**

1. Dhambi ni nini? 1 Yohana 3:4.
2. Ni nini Mshahara wa dhambi? Warumi 6:23.
3. Je, watenda dhambi wataridhi Ufalme wa Elohim? 1 Wakorintho 6:9-10.
4. Elohim alimwambia Kaini nini kuhusu dhambi? Mwanzo 4:7.
5. Kwa nini Elohim aliwaangamiza wenyeji wa Sodom na Gomorrah? Mwanzo 13:13, 19:1-25.
6. Ayubu alinena vipi kuhusu dhambi? Ayubu 10:6.

7. Ni nini kitafanyika kwa watenda dhambi? Waebrania 10:26-27.

## SOMO LA WATOTO LA OKTOBA 14, 2023
## AMRI

**Somo kuu : Kumbukumbu la torati 5:1-22**
**Fungu la kukariri : Ufunuo 14:12**

1. Nani alipeana amri kumi? Kutoka 20:1-4
2. Nani aliziandika amri kumi? Kutoka 31:18
3. Je,mwokozi wetu alizitupilia mbali amri kumi alipokuja ulimwenguni? Mathayo 5:17-18

4. Tukizitunza amri kumi, je tutapata uzima wa milele? Mathayo 19:16-17
5. Je tumeruhusiwa kuzivunja baadhi ya amri kumi? Yakobo 2:10-11
6. Nani wataruhusiwa katika mji ule mtakatifu? Ufunuo 22:14
7. Nani watakatifu? Ufunuo 14:12

## SOMO LA WATOTO LA OKTOBA 21, 2023
## KUTII

**Somo kuu : I Samueli 15:1-35**
**Fungu la kukariri : 1 Samueli 15:22**

1. Elohim huona uasi kivipi? 1 Samueli 15 :23

2. Ili tumfurahishe Elohim twafaa tufanye vipi? 1 Samueli 15:22
3. Je,manabii walimtii Elohim? 1 Samueli 3:10,Hosea 4:2-3
4. Je, Masihi alipata kibari cha kupendwa na Elohim pamoja na watu kwa sababu ya kuwa mtiifu? Luka 2:52
5. Je,watakatifu wameamuriwa kutii Elohim kwa njia ya kuzitunza amri zake? Ufunuo 14:12
6. Ni kwa njia ipi twaweza kuonyesha upendo wetu na utiifu kwa Elohim? Yohana 14:15.
7. Je,watoto wameshauriwa kuwatii wszazi wao? Waefeso 6:1

## SOMO LA WATOTO LA OKTOBA 28, 2023
## MITUME WA MASIHI

**SomoKuu: Mathayo10:1-16**
**FunguLa Kukariri: Mathayo10:2-4**

1. Majina ya mitume wa Masihi ni yapi? Mathayo 10:2-4
2. Wakati Masihi alipowatuma, aliwaambia vipi kuhusu ufalme wa mbinguni? Mathayo 10:7
3. Ni nguvu ipi walipewa? Mathayo 10:8
4. Kwa hao mitume wake niyupi alimsaliti? Mathayo 10:4
5. Nani alirudi mahali pa yule aliyemsaliti? MatendoyaMitume 1:26
6. Baada ya Masihi kupaa mbinguni, je mitume wake waliendelea kuponya wagonjwa? Matendo ya Mitume 5:15
7. Kama wafuasi wa Masihi je tutapewa nguvu za uponyaji kam awalivyopewa? Mariko 16:17-18

## SOMO LA WATOTO LA NOVEMBA 4, 2019
## UBATIZO

**Somo kuu : Yohana 3:1-12**
**Fungu la kukariri : Yohana 3:3**

1. Masihi alinena vipi kuhusu ubatizo? Yohana 3:3.
2. Mitume walibatiza vipi? Matendo ya Mitume 2:38,19:5.
3. Je, Masihi alibatiza watoto? Mathayo 19:13-15.
4. Masihi alipokuwa mtoto, je alibatizwa? Luka 2:25-29.
5. Mtu hubatizwa kwa njia gani? Mathayo 3:16,Warumi 6:3-4
6. Ni aina ngapi za ubatizo hupatikana katika bibilia? Waefeso 4:5
7. Baada ya kubatizwa twaweza kutenda dhambi kisha tubatizwe tena? Waebrania 10:26-29

## SOMO LA WATOTO LA NOVEMBA 11,2023
## KUISHI KAMA MASIHI

**Somo Kuu: Luka 2:40-52**
**FunguLa Kukariri: Wafilipi 2:5**

1. Je, mitume waMasihi walimuiga? 1 Wakorinitho 11:1
2. Je, Masihi alizishika amri? Yohana 15:10
3. Ombi la Masihi kwa wafuasi wake lilikuwa lipi? Yohana 17:9
4. Maisha yake yalikuwa vipi? Alipokuwa mtoto mdogo? Luka 2:52
5. Ni ombi lipi aliwafunza wafuasi wake? Mathayo 6:9-14
6. Je, wafuasi wake watapata faida nyingi wakiishi ndani yake? Yohana 15:5
7. Nini anaahidi kwa wale watakaoishi kama alivyoishi? Ufunuo 3:21

## SOMO LA WATOTO LA NOVEMBA 18, 2023
## AMRI YA TANO

**Somo kuu: Kutoka 20:1-17**
**Fungu la kukariri : Kutoka 20:12**

1. Ni Amri ipi ya Kwanza yenye ahadi? Waefeso 6:1-2
2. Ni ahadi ipi? Waefeso 6:3
3. Ni vipi inastahili kumchukulia mtu mwenye umri sawa au mzee kuliko baba yetu mzazi? 1 Timotheo 5:1(sehemu ya Kwanza).
4. Ni vipi inastahili kumchukulia mtu mwenye umri sawa au mzee kuliko mama yetu mzazi? 1 Timotheo 5:2(sehemu ya Kwanza).
5. Tukitii wszazi wetu, je yaonyesha twampenda Elohim? Yohana 14:15
6. Je,Masihi aliitii amri hii alipokuwa mtoto? Luka 2:51
7. Ni vingumu kuitunza amri hii? 1 Yohana 5:3

## SOMO LA WATOTO WA NOVEMBA 25, 2023
## PAULO YULE MTUME

**Somo Kuu: MatendoYa Mitume 9**
**Fungu La Kukariri: Matendo Ya Mitume9:22**

1. Kabla ya kubadilika, Paulo alikuwa akifanya nini? Matendo ya Mitume 9:1-2
2. Nini kilifanyika kwake alipokuwa akisafiri kuenda Damesiki? Mtendo ya Mitume 9:3-4
3. Ni maneno yapi aliyasikia alipoanguka chini? Matendo ya Mitume 9:4
4. Ni Nani alikuwa ananena maneno hayo? Matendo ya Mitume 9:5

Ni Nani alitumwa kumuombea iliapate kuona tena? Matendo ya Mitume 9:10-12
6. Jina lake lilikuwa lipi kabla ya kubadilika? Mtendo ya Mitume 9:11
7. Ni kazi ipi alifanya ya kueneza injili? 1 Timotheo 2:7

## SOMO LA WATOTO LA DESEMBA 2, 2023
## AMRI YA SITA

**Somo kuu : Kutoka 20:1-17**
**Fungu la kukariri : Kutoka 20:13**

1. Amri ya Sita, inatuamuru nini? Kutoka 20:13
2. Nani alituamuru tusiue? Kutoka 20:1-13
3. Masihi alinena vipi kuhusu amri hii? Mathayo 5:21-22
4. Yohana yule mtume alinena vipi kuhusu amri hii? 1 Yohana 3:15
5. Mtu akiwa muuaji, baba yake ni nani? Yohana 8:44
6. Ili tusiwe wauaji, twafaa tufanye nini? Yohana 13:34
7. Je,muuaji ana uzima wa milele ndani yake? 1 Yohana 3:15

## SOMO LA WATOTO LA DESEMBA 9, 2023
## JE, MTU MTAKATIFU AKIFA, HUENDA MBINGUNI?

**Somo Kuu: Waebrania 11:1-40**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 11:39**

1. Je Habili alihesabiwa kuwa mwenye haki baada ya kutoa Sadaka? Waebrania 11:4
2. Je, alipokufa, aliendaMbinguni? Mwanzo 4:9-10
3. Paulo anasema vipi kuhusu wenye haki, watafufuka au wameshafufukatayari? MatendoyaMitume 24:15
4. Masihi alisema vipi kuhusu wale waliokufa wakiwa watakatifu? Yohana 5:28-29
5. Katika Kitabu cha Danieli, watakatifu wako wapi? Danieli 12:2
6. Waliokufa katika Masihi parapanda itakapolia watatokea wapi? 1 wathesalonike 4:16
7. Wakati Paulo alimaliza maisha yake, je aliahidiwa kuenda mbinguni? 2 Timotheo 4:7-8

## SOMO LA WATOTO LA DESEMBA 16, 2023
## JE, MTU MWENYE DHAMBI AKIFA, HUENDA KWENYE ZIWA LA MOTO?

**Somo Kuu: Ufunuo 20**
**Fungu La Kukariri: Matendo Ya Mitume 24:15**

1. Waliokufa wakiwa wenye dhambi wako wapi? Ufunuo 20:4-5
2. Tunaona wakitoka wapi ili wahukumiwe? Ufunuo 20:13-15
3. Je, mwenye dhambi aweza kutubu baada ya kufa? Zaburi 6:5
4. Mhubiri ananena vipi kuhusu jambo hili? Mhubiri 9:10
5. Ayubu anesema watu huenda wapi wakifa? Ayubu 14:10-12
6. Huwa tunasoma vipi katikaWaebrania 6:2? Waebrania 6:2
7. Mtu alikuwa aende wapi akifa? Mwanzo 3:19

## SOMO LA WATOTO LA DESEMBA 23, 2023
## UNABII WA BIBLIA

**Somo Kuu: 2 Petero 1:19-21**
**Fungu La Kukariri: Amosi 3:7**

1. Je, tunaweza kutafsir iunabii katika bibilia tukitumia hekima yetu? 2 Petero 1:20
2. Katika unabii Maji yanasimamia nini? Ufunuo 17:15
3. Mnyama au Wanyama inasimamia nini? Danieli 7:17
4. Mwanamke anasimamia nini? Waefeso 5:23-32
5. Upepo unasimamia nini? Yeremia 23:19
6. Ufunuo ulipewa nani? Ufunuo 1:1
7. Je, kuna baraka ya kusoma, kusikiza na kutunza maneno ya unabii? Ufunuo 1:3

## SOMO LA WATOTO LA DESEMBA 30, 2023
## KUJA KWA MASIHI MARA YA PILI

**Somo kuu : Matendo ya Mitume 1:1-12**

**Fungu la kukariri : Matendo ya Mitume 1:11**

1. Je, Masihi atarudi tena Mara ya pili? Waebrania 9:28
2. Je,aliahidi kuja tena mara ya pili? Matendo ya Mitume :1:11

3. Ni nini alimwambia mmoja wa mitume wake kuhusu Kuja kwake mara ya pili? Yohana 14:1-3
4. Atakapokuja mara ya pili, je tutatawala naye? Ufunuo 20:4
5. Nabii Zekaria amenena vipi kuhusu kuja mara ya pili kwake Masihi? Zekaria 14:1-9

6. Watu wote wenye watakuwa hai atakaporudi mara ya pili, je wote watamuona? Ufunuo 1:7
7. Nini kitafanyika kwa wale waliokufa wakiwa ndani yake? 1 Wathesalonike 4:16-17